

Maswali

1. Waisraeli walikuwa wanaenda kukamata mji gani?
2. Mbona Yoshua alituma watu wachache tu?
3. Mbona walishindwa kwa vita?
4. Huyu mtu aliiba nini?
5. Mungu alionyesha mtu aliyekosa namna ani?
6. Alitoka kwa kabila gani?
7. Nani alifanya dhambi?
8. Adhabu yake ilikuwa nini?
9. Waisraeli walichukua Ai namna gani?
10. Tunajifunza nini kwa hadithi hii?

Majibu

1. Ai
2. Wapelelesi walisema ni watu wachache walitakiwa kwa sababu ni mji mdogo.
3. Muisraeli mmoja hakutii Mungu.
4. Nguo nzuri, dhahabu na fedha
5. Kwa kutenga kabila yake, jamii yake, familia yake na mwishowe yeye mwenyewe.
6. Yuda.
7. Achani.
8. Familia yake yote ilipigwa kwa mawe halafu wakachomwa kwa moto.
9. Waliwavizia kwa siri.
10. Lazima tumtii Mungu kwa sababu anajua matendo na mawazo yetu yote.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 2



11 Hadithi ya Ai na Achani

Marejeo

Yoshua 7: 1—5, 10—11 & 16—26; 8: 3—8

Kiini cha somo

Mungu wakati wote hujua tunachofanya hata tukificha dhambi zetu kwa wenzetu.

Maneno maalum

1. Yoshua + Ai
2. Fukuza + omba + nguo nzuri + kosa
3. Kabila + familia + piga mawe + choma
4. Usiku + jifija + moshi inatoka + danganya + amini


11.1 Waisraeli watu wateule wa Mungu walijaribu kuchukua nchi yao waliyoahidiwa na Mungu. Kiongozi wao Yoshua alituma watu kupeleleza Ai. Walirudi na kuambia Yoshua kwamba ni watu wachache tu walitakiwa kuenda kupigana ili wachukue Ai, kwa sababu haukukuwa mji mkubwa.

11.2 Waisraeli walienda kupigana na watu wa Ai wakidhani itakuwa rasi kushinda. Lakini wengi wao waliuwawa na wengine wakafukuzwa kutoka mjini. Yoshua alifadhaika na akaomba mpaka jioni. Hata wakuu wao walifanya hivyo. Yoshua aliuliza Mungu sababu gani hawakutwaa huo mji. Mungu alimwambia kwamba hakukuwa nao. Muisraeli mmoja hakumtii Mungu. Alikuwa ameiba baadhi ya nguo nzuri, dhahabu na fedha kutoka kwa mji walioutwaa na hali walikuwa wamekatazwa na Mungu. Na Mungu angemwonyesha vile atamjua huyo mtu aliyekosa.



11.3 Israeli ilikuwa na kabila 12 tofauti. Mungu alionyesha kwamba yule mtu anatoka kwa kabila la Yuda. Tena akatoa jamii ya Wazera. Kutoka kwa hii jamii alitua familia ya Zabdi. Kufikia hapa, lazima yule aliyekuwa amekosa alingiwa na uoga sana. Mmoja baada ya mwingine watu wa hiyo familia walijitokesha na Mungu akaonyesha huyo mkosaji. Alikuwa Achani. Yoshua alimwambia Achani atubu hiyo dhambi. Achani aliwaelezea vile alichukua hivyo vitu na akatubu dhambi yake. Kuaadhibi Achani na familia yake, walipigwa kwa mawe na baadaye wakachomwa moto.

11.4 Mungu alimwambia Yoshua ajaribu kuchukua Ai tena na wakati huu Mungu atakuwa nao. Yoshua alituma wapiganaji wazuri usiku na wakajificha nyuma ya Ai. Lakini watu wachache walienda na Yoshua mpaka mjini. Watu wa Ai waliwafukuza. Walipokuwa wakiwafukuza, waliochificha walitoka na kuwasha mji wa Ai kwa moto. Watu wa Ai walipoona moshi unaenda juu, walijua wamedanganywa. Yoshua na watu wake waligeuka na kuanza kupigana nao. Watu wa Ai walishambuliwa kutoka pande zote. Waisraeli waliua watu wa Ai wote na kutundika mfalme mtini. Wakati Waisraeli waliamini Mungu, Mungu aliwasaidia.



11.5 Hadithi hii inatufundisha umuhimu wa kutii Mungu. Anajua yote tunayofanya na tunayofikiria. Hata tukijifija kwa rafiki na familia zetu, kwa Mungu hatuwezi.